**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI-TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU**

**SHULE YA SEKONDARI YA MWANZA GIRLS**

**SIMU 0760672234 P.O.BOX 200 MAGU BARUA**

**PEPE mwanzagirls@gmail.com**

KUMB.BGSS/JIF/01/2024

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi

…………………………………………..

S.L.P………………………………

………………….…………….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA MWANZA GIRLS KWA MWAKA WA MASOMO ………………………………**

Mpendwa mwanafunzi…………………………………………………………

**1.0 UTANGULIZI**.

Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na **kidato chaTano** mwaka wa masomo **……………………………** katika shule ya sekondari ya wasichana Mwanza Girls.

**A: Mahali shule ilipo**

Shule ya sekondari ya MWANZA GIRLS' ipo mkoani **Mwanza** wilayani **Magu** kata ya **Bujashi** umbali wa **km 6** kutoka **Kisesa kona ya Kayenze** ambayo iko umbali wa **km 18** kutoka **Mwanza mjini.** Aidha**,** Iwapo umetokea stendi kuu ya mabasi Nyegezi au stendi ya mabasi Nyamhongolo panda daladala au coaster ziendazo Kisesa mwambie kondakta akushushe stendi ya Kisesa (Kona ya Kayenze) ndiyo mwisho wa daladala hizo.Hapo utachukua bodaboda au bajaji kufika shule ilipo kupitia barabara ya Kayenze karibu na shule ya sekondari Bujashi. Na iwapo umetokea Magu mjini panda daladala,Coaster au Tata mwambie kodakta akushushe stendi ya Kisesa kona ya Kayenze.Hapo utachukua bajaji au bodaboda kufika shule ilipo barabara ya Kayenze karibu na shule ya sekondari Bujashi. Nauli kutoka mjini ni Tsh 1000= kwa daladala/coaster na Tsh.2000= kwa pikipiki/bajaji toka kona ya kayenze

Masomo ya taanza **TAREHE ……………. .** **hivyo** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia **TAREHE ...............................** kabla ya saa 11 hawakupangiwa shule katika awamu hii.

Pamoja na barua hii naambatanisha orodha ya vifaa muhimu ambavyo lazima uwe navyo, sheria za shule, kanuni za shule ambazo unatakiwa uzifuate kwa muda wote utakaokuwa mwanafunzi wa shule hii, **nakala ya cheti cha kuzaliwa kama hauna uje na Affidavity . Fomu ya uthibitisho wa afya yako iliyojazwa na daktari wa hospitali ya serikali tu**, fomu ya taarifa binafsi ambazo unatakiwa kuzikamilisha kabla hujafika shuleni, nakala ya result slip/nakala ya hati ya matokeo original na fotokopi pamoja na fomu ya kukubali nafasi ya shule. Mzazi/mlezi na mwanafunzi, mnatakiwa kusoma/kujaza maelekezo hayo kwa makini ilikuepusha usumbufu unaowezakuji tokeza.

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MWANZA
S.L.P. 200
MAGU - MWANZA

**Mecktilda J. Shija**

**MKUU WA SHULE**

**B. MICHANGO**

**Michango ifuatayo ilipwe kwenye akaunti 0150770047800 CRDB. Jina la akaunti MWANZA GIRLS SECONDARY SCHOOL-RECURRENT ACCOUNT.**

| NA. | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| **1** | **Mchango wa uendeshaji shule** | **65,000/=** |
| **2** | Tahadhari | **5,000/=** |
| **3** | Nembo | **5,000/=** |
| **4** | Kitambulisho cha shule | **5,000/=** |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB**:

a.Tafadhali unakumbushwa kulipa kwa kuzingatia namba za akaunti ulizopewa.

b. Hapa shuleni hatupokei pesa taslimu, Ada na michango yote elekezi ni lazima ilipiwe Benki isipokuwa pesa ambayo mzazi ameelekezwa kuwa iletwe mkononi tu.

c. Risiti ya malipo halisi (original) iletwe shuleni mwanafunzi atakaporipoti

d) Malipo yote ya bank yaanze kuingizwa tarahe **............................** na si kabla ya hapo

**C: SARE ZA SHULE**

1. Sketi mbili zikiwa namarinda mapana, na rinda box moja rangi ya dark blue ndefu kitambaa cha suti urefu katikati ya magoti na makanyagio (kwa atakayehitaji kununua shuleni zinapatikana)
2. Shati mbili nyeupe za mikono mirefu kitambaa cha cotton
3. Vazi la kiislam linalotumika kama sare ya shule liwe n akitambaa cha kichwani cheupe, (juba) nusu kanzu nyeupe kitambaa cha cotton na suruali dark blue kitambaa cha suti (kwa atakayehitaji kununua shuleni inapatikana)
4. Gauni mbili zenye rangi ya light blue ndefu kwenda chini katikati ya magoti na makanyagio (kwa atakayehitaji kununua shuleni inapatikana)
5. Vazi la kiislamu linalotumika kama nguo ya kushindia (shamba dress) liwe la rangi ya light blue. (gauni refu na kitambaa cha kichwani) (kwa atakayehitaji kununua shuleni inapatikana shuleni)
6. Sweta moja dark blue (kwa atakayehitaji kununua shuleni inapatikana shuleni)
7. Shuka mbili rangi ya pink na foronya zake
8. Tai moja dark blue yenye mistari mshazali mieupe (kwa atakayehitaji kununua shuleni inapatikana shuleni)
9. T-shirt moja yenye kola shingoni rangi ya light blue (kwa atakayehitaji kununua shuleni inapatikana shuleni)
10. Track suit nyeusi, viatu raba na jezi nyeusi kwa ajili ya michezo (kwa atakayehitaji kununua shuleni inapatikana shuleni)
11. Open shoes, viatu vya Ngozi vya kufunika

**ANGALIZO**: Mavazi yote inabidi yawe yenye hadhi, ukishindwa kuelewa maelekezo haya unaweza kupata huduma hizo hapa shuleni kwani wapo mafundi wanafanya kazi hizo kwa gharama za kawaida. Soma kiambatanisho cha bei ya sare, sare isiyo zingatia maelekezo haitapokelewa

**D : VIFAA NA MAHITAJI MENGINE:**

1. Chandarua (nyeupe)
2. Ndoo mbili (2) ndogo (lita kumi) zenye mifuniko. Pia alete chombo cha kuhifadhia maji safi ya kunywa.
3. Vifaa vya usafi binafsi kama pedi, miswaki na dawa, sabuni, mafuta, toilet paper n.k.
4. Vifaa vya kulia chakula – kikombe, sahani, kijiko pamoja na bakuli lenye mfuniko.
5. Viatu vya wazi (sandal) kwa kushindia
6. Ream mbili**(2)** za karatasi **(photocopy paper, - A4ainaya Double A).**Mwanafunzi atatakiwa kuleta ream mbili kila mwaka – iletwe muhula wa kwanza

7. Soksi ndefu nyeupe zisizo na maua jozi mbili, viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na urembo - visigino vifupi, kiwi na brashi.
8. Raba kwa ajili ya michezo.
9. Gun boot

10. Madaftari makubwa ya kutosha masomo yake yasiyopungua 10
11. Vifaa vya somo la hisabati (Mathematical set), Calculator(**Scientific calculator FX 991 ES made in Thailand** ), graph pad 1 pamoja na **DISECTING – KIT 1** kwa wanafunzi wanaosoma somo la **Biolojia.**
12. Tochi 01 inayotumia mwanga wa jua kwa matumizi binafsi
13. Mashuka mawili ya pink , mto mmoja na blanketi moja zito.
14. Godoro **lenye vipimo vya 3x4x6. Liwe jipya**
15. Nguo za ndani za kutosha kama chupi, gagulo shimizi, skin tight n.k – ziwe nyeupe au nyeusi, taulo, khanga/vitenge
16. Kila mwanafunzi aje na mifagio miwili **(02)** ya chelewa **,**ndoo moja kubwa**(1)** na ndoo moja ndogo**(1)** pamoja na:-

- Jembe 1, *kwa wanafunzi wa PCB*
- *Fyekeo 1, kwa wanafunzi wa CBG*
- Reki 1, kwa wanafunzi wa wa PCM
- Soft broom na squizer kwa wanafunzi wa HGL
- Hard broom na squizer kwa wanafunzi wa HKL

**Muhimu:**

1. Fedha anazotumiwa mwanafunzi akiwa shuleni zitumwe kwa njia ya M-PESA namba 0**760672234** -**MECKTILDA SHIJA.** Mzazi akishatuma fedha hiyo atume ujumbe kwenye simu namba(**0760672234)** akiandika jina la mwanafunzi aliyemtumia fedha hiyo, ukionesha jina la mwanafunzi darasa na tahasusi anayosoma. Mwanafunzi hataruhusiwa kwenda BENKI, POSTA/KITUO CHA MABASI kuchukua fedha zitakazotumwa kwa njia hizo. Uongoziwa Shule hautahusika na miamala ya fedha itakayofanyika kinyume na utaratibu uliotolewa Unashauriwa kumnunulia mwanao vitabu kulingana na masomo anayosoma.
2. Wanafunzi wote wanatakiwa kuripoti shuleni mapema kuanzia saa1**.30** asubuhi mpaka saa**9.30.** jioni. Mawasiliano yote yakiofisi kwa njia ya simu itumike namba **0760672234**. Muda wakazina siku za kazi tu.

**2.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi naTechonoljia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na:-

2.1 **Sheria na Kanuni za Shule**

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
3. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (preparation)
4. Kuwa hikatika kila shughuli za shule utakazopewa.
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
6. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
7. Kuvaa sare ya shulewakatiwoteunapotakiwa .
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
9. Kutunza mali za shule.
10. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari
11. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa mkuu wa shule. (msiba au ugonjwa)**

**2.2 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI PAMOJA NA: -**

1. Wizi
2. Kutokuhudhuria masomo zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro
3. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
5. Kupiga na mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule
6. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule
7. Ulevi au unywajiwa pombe na matumizi ya dawa za kulevya
8. Uvutaji wa sigara.
9. Uasherati, mahusiano ya jinsia moja, kuoa au kuolewa na ushoga

10. Kupata ujauzito au kutoamimba
11. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
12. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
13. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
14. Kudharau benderaya Taifa
15. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kama kunywa sumu.
16. Uharibifu wa mali za umma kwa makusudi.

**A*: MAHUDHURIO:***

Kila mwanafunzi anatakiwa,

1. Kuhudhuria shule muda wote wa masomo.
2. Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
3. Kuhudhuria katika kazi zote za mikono.
4. Kuhudhuria mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa, mikutano ya nyumba(mabweni) na madarasa.

**B.: MAANDALIO YA JIONI:**

1. Kila mwanafunzi anatakiwa ahudhurie maaandalio ya jioni **1:30** hadi saa **4:00** usiku.
2. Ili kufanikisha maandalio ya jioni, kila mwalimu wa somo atakuwa anatoa kazi na

Kuhakikisha kuwa kazi hizo zimefanywa.

3. Walimu wazamu watakuwa wanasimamia maandalio ya jioni kikamilifu.

**C: KUWAHI:**

Kila mwanafunzi anatakiwa:-

1. Kuthamini muda
2. Kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba yakila siku.
3. Kufika shuleni kwa tarehe zilizopangwa.

**NB:**Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa kofia, viatu vyenye visigino virefu, mapambo yoyote pamoja na sare za shule.

**D: SARE ZA SHULE:**

kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare ya shule wakati wote wa:-

1. Masomo darasani
2. Kutoka nje ya shule kwa shughuli za kishule
3. Kwenda hospitali
4. Baraza la shule

5. Anaposafiri kuja shuleni au kwenda nyumbani kwao wakati wa likizo
6. Kazi za mikoni (**vazi la kazi**)
7. Michezo

***NB:*** mwanafunzi haruhusiwi kuvaa kofia ,viatu vyenye visigino virefu ,mapambo yoyote pamoja na sare za shule .

**F: MIPAKA YA SHULE:**

Kila mwanafunzi azingatie mipaka ya shule kama ifuatavyo:-

1. Kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mkuu wa shule.
2. Kutotembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalumu

a) Ofisi ya walimu (staff room)

b) Ofisi nyingine za shule

c) Maabara

d) Jikoni

e) Nyumba za walimu/wafanyakazi wasio walimu.

**G: UGONJWA:**

**1.** Mwanafunzi mgonjwa ataruhusiwa kupumzika katika /zahanati ya shule na

Endapo atazidiwa atapelekwa katika **Hospitali** ya **Serikali.**

2. Mwanafunzi mwenye matatizo lazima amfahamishe **Matron/ Mama malezi** wa shule, mara afikapo shuleni.
**3.** Mwanafunzi aje na bima ya afya inayotumika au aje na tsh. 50,400/= kwa ambaye hatakuwa na bima.

**3.0 VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU.**

1. Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali Ya Serikali
2. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwnafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
3. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa nashule
4. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wakaribu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

## SHULE YA SEKONDARI MWANZA GIRLS

## FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MWANZA.

1. **Sehemu ya Mwanafunzi:**

Mimi …………………………………………..Ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha **tano** mwaka ……………… katika shule ya sekondari ya Wasichana Mwanza nanitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shulena za nchi.

Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za Elimu ya kujitegemea. Nitariporiti shuleni kwa muda uliopangwa kila ninapofunga likizo

Anuani yangu ya kudumu ni: ……………………………

………………………………

………………………………

**2: SehemuyaMzazi/Mlezi.**

Mimi……………………………………… ninakubali mtoto wangu ………………………………..kuchukua nafasi kuingia Sekondari ya Wasichana Mwanza. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule na atafika shuleni kwa tarehe iliyopangwa kila wakati. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa Taifa. Nitahakikisha mwanangu anaripoti shuleni kwa wakati kila muhula shule inapofunguliwa. Anuani yangu ya kudumuni:

……………………………………………………………….

…………………………………………………

Iwapo nitahamishwa au kubadili makazi, nilazima nitaijulisha shule kwa maandishi.

**SEHEMU A: TAARIFA BINAFSI**

1. JINA KAMILI LA MWANAFUNZI……………………………………………………………………………….
2. TAREHE YA KUZALIWA…………………………………………………………
3. SHULE YA MSINGI ALIKOSOMA…………………………………………………
4. SHULE YA SEKONDARI ALIKOTOKA……………………………………
5. TAHASUSI/COMBINATION ANAYOSOMA……………………………………………………….

**SEHEMU B: TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

6. JINA LA MZAZI/MLEZI……………………………………………………………..
7. MAHALI ANAPOISHI
8. MTAA/KIJIJI………………………………………….
9. WILAYA…………………………………………
10. MKOA……………………………….
11. NAMBA YA SIMU…………………………………………

# MEDICAL EXAMINATION FORM

Mwanza Girls' Secondary School

P.O. BOX 200

**MAGU.**

……………………………

**Ref. No. BGSS/**

The Medical Officer
…………………………………………….
……………………………………………
…………………………………………….
Please examine ……………………………………………………………………………. as to her fitness for pursuing advanced Secondary Education at this School.

1. Hemoglobin……………………………………………………………………………………………………

2. P.V.Bleeding……………………………………………………………………………………………………

3. (a)Sight…………………………………………………………………………………………………………..

4. (b)Hearing………………………………………………………………………………………………………
5.BloodPressure……………………………………………………………………………………………..
6. SickleCellTest……………………………………………………………………………………………………
7. Deformit…………………………………………………………………………………………………………
8. Urine for sugar & Pregnancy test……………………………………………………………………..
9. Epileps……………………………………………………………………………………………………………
10. Leprosy………………………………………………………………………………………………………….
11. Heart Examination ………………………………………………………………………………………
12. Tumors - breast………………………………………………………………………………………………
13. Pulmonary tuberculosis ………………………………………………………………………………
14. Stool for routine Examination ……………………………………………………………………..
15. Asthma ……………………………………………………………………………………………………………
16. Skin diseases……………………………………………………………………………………………………

**Comments**

……………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………

**NAME: ………………………………… SIGNATURE ………………… DESIGNATION………………………**

**STATION:………………………… OFFICIAL STAMP……………………......DATE:……………………**

**SHULE YA SEKONDARI MWANZA GIRLS**

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE**

**1.** Jina kamili (Kama ilivyo kwenye *SEL - FORM*) ....................................................................

**2.** Anwani ya nyumbani S.L.P ……………………………. WILAYA ………………………………..

**3.** Tarehe ya kuzaliwa ………………………………………………………………………………………………….

**4.** Mahali ulipozaliwa, Kijiji ………………………………. Kata ……………………………………. Tarafa …………….

**5.** Mahali unapoishi kwa sasa ………………………………………….. WILAYA ……………….

**6.** Shule ya sekondari ulikotoka……………………………......Anwani…………………………

**7.** Dini/Dhehebu ………………………………...................... Kabila …………………………

**8.** Jamaa katika familia ambao wanaweza kupelekewa taarifa muhimu kwa masuala yahusuyo shule:

**(i)** Jina la Baba ………………………………………………. Namba ya simu ……..........................
Hai/Si hai …………………… (kama hai) kazi yake ……......................... Anwani …………..

**(ii)** Jina la mama ……………………………………………... Namba ya simu ...............................
Hai/Si hai…………………… (kama hai) kazi yake ……...................... Anwani ………......

**(iii)** Jina la Mlezi ………………………………. Uhusiano …………………… Namba ya simu ……….................. kazi yake …………………………… Anwani S.L.P………………..
WILAYA ………………………………….

**(iv)** **(iv)** Jina la Mlezi ………………………………… Uhusiano ……………………………
Namba ya simu ……….................. kazi yake ………………...............
Anwani S.L.P…………………….. WILAYA ………………………………….

**NB: BANDIKA PICHA ZA WANAOHUSIKA HAPO JUU KWENYE VIBOMA**

| PASIPOTI BABA | PASIPOTI MAMA | PASIPOTI MLEZI | PASIPOTI MLEZI |
|---|---|---|---|

SIMU …………………………… ……………………….. …………………………… ……………………..

**FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YANAYOTOLEWA NA SHULE**

Mimi (Mwanafunzi) …………………………………………………………………………… nathibitisha kuwa taarifa nilizozijaza hapo juu ni za kweli. Ahadi yangu nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii na ninaahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule.

……………….................. ……………………

**Saini ya Mwanafunzi** **Tarehe**

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi) ……………………………………………………… Ambaye ni Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............................................................ nimeyasoma masharti na sheria za shule ya Sekondari MWANZA GIRLS ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoelezwa. Aidha, naahidi kushirikiana na uongozi katika malezi bora ya mwanangu ili baadaye awe raia bora na mwema wa Taifa letu.

………………………………………………….. ………………………

**Saini ya Mzazi/Mlezi** **Tarehe**

**KIAMBATANISHO**

**SARE ZA SHULE ZINAZOSHONWA HAPA SHULENI NA GHARAMA ZAKE**

| S/N | AINA YA SARE | KIASI (SH) | IDADI | JUMLA (SH) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Sketi | 25,000/= | 2 | 50,000/= |
| 2. | Gauni la kushindia | 20,000/= | 2 | 40,000/= |
| 3. | Hijab (sare ya kiislamu)ya darasani | 33,000/= | 2 | 66,000/= |
| 4. | Hijab (sare ya kiislamu)ya kushindia | 30,000/= | 2 | 60,000/= |
| 5. | T.  shirt | 10,000/= | 1 | 10,000/= |
| 6. | Tai | 5,000/= | 1 | 5,000/= |
| 7 | Truck suit | 30,000/= | 1 | 30,000/= |
| 8. | Sweta | 15,000/= | 1 | 15,000/= |
| 9 | Jezi | 16,000/= | 1 | 16,000/= |
| 10 | Shati | 15,000/ | 2 | 30,000/= |
| 11 | Shuka | 15,000/= | 2 | 30,000/= |

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

Saini ya mkuu wa shule ……………………………….

Jina la mkuu wa shule…………………………………..

Muhuri wa mkuu wa shule…………………………..

**NB**: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mtandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI / MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-

- Mkuu wa shule **0768105363**
- Makamu mkuu wa shule **0718782835**
- Mwandamizi taaluma **0766889938**